THE REGISTERED TRUSTEES OF WATER TECHNICIANS FUND

C/o Water Institute; P.O Box 35059 Dar es Salaam,

Tel: +255 (0)22-24100410; Mobile: +255 0718 432360

Email: info@rtwtf.or.tz; website: www.rtwtf.or.tz

24 Aprili 2017

MAOMBI YA MKOPO KWA WANAFUNZI WAPYA NA WANAOENDELEA

The Registered Trustees of the Water Technicians Fund (RTWTF) inawatangazia kutuma maombi kwa wanafunzi wote wenye uhitaji wa mkopo ambao wanategemea kudahiliwa na wanaoendelea na masomo katika Chuo cha Maji ngazi ya cheti na stashahada kwa mwaka wa masomo 2017/2018.

Wanafunzi wenye uhitaji wa mkopo kwa ajili ya masomo kwa mwaka 2017/2018 wanaelekezwa kusoma na kuzingatia muongozo ambao umeainisha vigezo na masharti ya kupata mkopo. Aidha wanafunzi wanakumbushwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa na bodi kabla ya kuomba mkopo huu.

Fomu ya mkopo inapatikana katika tovuti ya RTWTF ambayo ni: www.rtwtf.or.tz na tovuti ya Chuo cha Maji ambayo ni: www.waterinstitute.ac.tz kuanzia tarehe 24 Aprili 2017 na mwisho wa kupokea fomu ni tarehe 30 Agosti 2017 saa 10:00 Jioni (kumi kamili).

MWONGOZO NA TARATIBU ZA KUTOA MKOPO KWA MWANAFUNZI KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018

UTANGULIZI

The Registered Trustees of the Water Technicians Fund (RTWTF) imesajiliwa Machi 2013 kwa dhumuni la kutoa mkopo kwa wanafunzi waliodahiliwa au wanaotarajia kudahiliwa na Chuo cha Maji. Kwa mujibu wa mwongozo wa RTWTF, anayestahili kuomba mkopo ni mwanafunzi aliyedahiliwa au anayeomba kudahiliwa na Chuo cha Maji. Mwombaji anaweza kupata mkopo katika mahitaji yote aliyoainisha kwenye fomu au baadhi ya mahitaji kwa kadri Bodi itakavyoona uhitaji wake.

Kifungu Na. 5.1 cha mwongozo wa RTWTF kinasema kwamba mwanafunzi anayeweza kupewa mkopo ni sharti:

- awe Mtanzania;
- awe amedahiliwa au anaye endelea na masomo akiwa na ufaulu unaomruhusu kwenda mwaka mwingine wa masomo;
- awe amejaza fomu kwa usahihi na kwa ukamilifu;
- awe mtu asiye na uwezo wa kujisomesha katika Chuo cha Maji;

- awe ametimiza vigezo vingine vilivyowekwa na Bodi ya mkopo ya RTWTF .

VIGEZO VYA MKOPO KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018

Wanaostahili kupewa mkopo kwa mwaka wa masomo 2017/2018 wawe wametimiza vigezo na masharti yafuatayo:

i) Awe Mtanzania
ii) Awe ameomba mkopo
iii) Awe amedahiliwa na Chuo cha Maji katika ngazi ya cheti au stashahada
iv) Awe anaendelea na amefaulu masomo yake kumwezesha kuingiza mwaka unaofuata wa masomo katika Chuo cha Maji
v) Asiwe na ufadhili wa masomo kutoka kwa serikali/ mtu/ kikundi au shirika lolote
vi) Asiwe mwajiriwa wa sehemu yeyote
vii) Wanafunzi wa kike wenye uhitaji wa mkopo wa masomo wanahamasishwa kuomba mkopo huu

VIGEZO VINGINE VYA MKOPO

RIBA YA MKOPO UNAOTOLEWA

Bodi ya RTWTF imeona ili mkopo uwe endelevu na wenye thamani utatozwa riba ya kiasi cha 6% kwa kila mwaka mwanafunzi apokeapo mkopo huu.

MAREJESHO YA MKOPO

Marejesho ya mkopo yanatakiwa kuanza mwaka mmoja baada ya mwanafunzi kumaliza masomo yake katika Chuo cha Maji.

JINSI YA KUOMBA MKOPO

Bodi ya RTWTF imeandaa fomu za mkopo na inawakaribisha wanafunzi wote wenye uhitaji wa mkopo kwa mwaka 2017/2018 kujaza fomu hizo na kuzipeleka ofisi ya RTWTF yenye majengo yake ndani ya Chuo cha Maji au kutuma kwa njia ya Posta. Hakikisha fomu imejazwa vizuri na viambatishi vyote vipo sahihi. Kwa wanaotuma kwa njia ya posta anwani ni:

Mwenyekiti,
The Registered Trustees of the Water Technicians Fund,
C/o Water Institute
S.L.P 35059,
Dar es Salaam.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na ofisi za RTWTF zilizopo Chuo cha Maji, barabara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuanzia saa 2:30 asubuhi mpaka 9:00 jioni (Jumatatu-Ijumaa).
Mwombaji anashauriwa kutunza nakala ya fomu na risiti kwa manufaa yake ya baadae.

ADA YA MAOMBI YA MKOPO

Waombaji wote wanatakiwa kuilipia fomu ya mkopo Sh. 15,000/=. Fomu iambatishwa na risiti ya malipo, vinginevyo haitashughulikiwa. Kabla ya kuiwasilisha au kuituma RTWTF, kiasi hiki huwa hakirudishwi hata kama ukikosa mkopo. Kiasi hiki kilipwe kwenye akaunti ya RTWTF ambayo ni:

Jina la Akaunti:	**Registered Trustee of Water Technicians Fund**
Namba ya Akaunti:	**0150316425200**
Benki:	**CRDB**
Tawi:	**Mlimani City**

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI YA MKOPO

Mwisho wa kupokea fomu za mikopo ni tarehe 30 Agosti 2017.

TANGAZO KWA WANAFUNZI WALIOFANIKIWA KUPATA MIKOPO

Orodha ya wanafunzi waliopata mkopo na kiasi walichopata kitawekwa kwenye tovuti ya RTWTF, Chuo cha Maji (Water Institute) na mbao za matangazo za Chuo cha Maji mara baada ya kumaliza uchambuzi wa kuwapata waliokidhi vigezo vya kupata mkopo.

Mwenyekiti wa Bodi

THE REGISTERD TRUSTEES OF THE WATER TECHNICIANS FUND

THE REGISTERED TRUSTEES OF WATER TECHNICIANS FUND

(MFUKO WA MIKOPO WA MAFUNDI SANIFU WA MAJI)

C/o Water Institute; P.O. Box 35059 Dar es Salaam,

Tel: +255 (0)22-24100410; Mobile: +255 0718 432360

Email: info@rtwtf.or.tz; website: www.rtwtf.or.tz

Na. ya mtihani kidato cha nne: Fomu na.

MAOMBI YA MKOPO KWA WANAFUNZI WA NGAZI YA CHETI NA STASHAHADA

(2017/2018)

MAELEZO BINAFSI NA ANWANI YA MWOMBAJI

Jina Kamili:……

Jinsia : ……

Tarehe ya kuzaliwa : ……

Mahali ulipozaliwa : ……

Mkoa ulikozaliwa : ……

Uraia : ……

Kazi ya mzazi/mlezi : …… ……

Namba ya simu ya mkononi ya mwanafunzi : ……

Barua Pepe (E-mail): ……

Namba ya usajili (WI Registration number): ……

Mwaka wa Masomo (NTA level): ……

Anuani ya Kudumu: ……

……

MAELEZO YA ELIMU YA MWOMBAJI

Elimu kabla ya kujiunga na Stashahada (Pre Diploma Education History)

Shule ya Sekondari Kidato cha 4 (O- Level Secondary School): ……

Namba ya Mtahiniwa (Form Four Index): ……...

Shule ya Sekondari Kidato cha 6 (A- Level Secondary School): ……

Namba ya Mtahiniwa (Form Six Index): …….

MAHITAJI YA MKOPO

Tiki kati ya sababu zifuatazo:

1. Naomba mkopo kwa ajili ya:

☐ Ada

☐ Chakula

☐ Malazi

☐ IPT

☐ Mengineyo (elezea) .....

2. Ufadhili wa masomo ulionao sasa:

☐ Binafsi

☐ Serikali

☐ Shirika

☐ Ufadhili mwingine (elezea) .....

SABABU ZA KUOMBA MKOPO

Tiki mojawapo kati ya sababu zifuatazo:

1. Sababu za kuomba mkopo huu

☐ Wazazi wote wawili hawapo hai na hakuna msaada mwingine wowote wa kujilipia

☐ Mzazi mmoja hayupo hai na hakuna msaada mwingine wowote wa kujilipia

☐ Wazazi wote wapo ila hawana uwezo (Elezea na ambatisha barua toka Serikali ya Mtaa)

☐ Sababu nyingine (Elezea na ambatisha barua toka Serikali ya Mtaa)

MASHARTI YA MKOPO KWA MWAKA 2017/2018

viii) Awe amejaza fomu yote na amekamilisha viambatanishi vyote kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 10

ix) Awe raia waTanzania

x) Awe ameomba mkopo

xi) Awe amechaguliwa kujiunga na Chuo cha Maji (WI) kusomea cheti au stashahada ya kozi zinazotolewa

xii) Awe mwanafunzi wa WI anayeendelea, ambaye amefaulu mitihani yake yote inayomruhusu kuendelea na masomo yake kwa mwaka unaofuata

xiii) Awe mtu ambaye hajapewa msaada wa kimasomo kutoka kwenye vyanzo vyovyote vingine

xiv) Asiwe mwajiriwa

UTHIBITISHO WA MWOMBAJI

Mimi..... ninatamka kuwa maelezo yaliyotolewa kwenye maombi haya kwa njia ya tovuti, ambayo sehemu yake yamechapwa hapa, kuwa ni ya kweli kwa kadri ya ufahamu wangu. Ninatamka pia kwamba ninafahamu kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yangu endapo itabainika kwamba maelezo niliyoyatoa sio sahihi ama yanapotosha.

Jina Kamili la Mwombaji: _____ Tarehe: _____ Sahihi: _____

UTHIBITISHO WA SERIKALI YA KIJIJI/MTAA KUHUSU MAELEZO YA MWOMBAJI

MAOMBI HAYA YATAKUWA BATILI ENDAPO HAYATAPITISHWA NA SERIKALI YA KIJIJI/MTAA

ANGALIZO: Kiongozi yeyote wa Serikali ya Kijiji au Mtaa atakayethibitisha maombi haya ya mkopo, ambaye ama kwa kujua au uzembe akashuhudia taarifa za uongo zilizojazwa na mwombaji na Wazazi wake atakuwa na hatia ya jinai na anaweza kutozwa faini isiyozidi shilingi Milioni moja na laki tano (1,500,000) au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja. Kughushi ni kosa la jinai na mtu anayegushi au kushuhudia makosa kama hayo atashitakiwa mahakamani.

1. Jina la Mzazi/ Mlezi: ……..
2. Kijiji/ Mtaa anachoishi Mzazi/ Mlezi: ……
3. Mzazi/ Mlezi ana watoto wangapi? ……
4. Mzazi/ Mlezi anajishughulisha na kazi gani: …….
5. Elimu ya Mzazi/ Mlezi: ……..
6. Je Mzazi/ Mlezi anamiliki wanyama wowote? Ndiyo ……., Hapana……...
7. Kama Mzazi/ Mlezi anamiliki wanyama toa idadi

Na	Aina ya Mnyama	Idadi ya Wanyama

8. Je Mzazi/ Mlezi anamiliki shamba au kiwanja? Ndiyo ……, Hapana …….

9. Ukubwa wa shamba au kiwanja ……

10. Je nyumba anayoishi Mzazi/ mlezi ni mali yao ….. au wamepanga …. (tiki kwenye jibu sahihi)

11. Toa maelezo kuhusu uchumi wa Mzazi/ mlezi wa mwombaji wa mkopo huu:

    ……

    ……..

Muhuri wa Serikali ya Kijiji/Mtaa

No	JINA KAMILI	CHEO	JINA LA MTAA/ KIJIJI	NAMBA YA SIMU	SAHIHI	TAREHE
1		Mwenyekiti Serikali ya Mtaa				
2		Mjumbe wa nyumba kumi/ Balozi				

8. Mwenyekiti wa kijiji/ Mjumbe wa nyumba kumi/ Mtaa yuko tayari kuisadia RTWTF katika kufuatilia uhakika wa taarifa za Muombaji: Ndiyo…… Hapana……

9. TAARIFA MUHIMU KWA MWOMBAJI WA MKOPO HUU:

Mkopo huu utatozwa asilimia sita (6%) kwa mwaka kama gharama ya kuhifadhi thamani ya fedha (value retention fee) zitakazokopeshwa ambazo zitalipwa pamoja na marejesho ya mkopo. Riba na

marejesho ya mkopo wa mwanafunzi yataanza kulipwa baada ya mwanafunzi kumaliza masomo na atapewa muda wa mwaka mmoja kama nafuu ndipo aanze kulipa mkopo. Endapo mwanafunzi atashindwa kulipa mkopo huu kwa muda wa miaka miwili mfululizo baada ya muda wa kulipa mkopo, Bodi ya mkopo itashirikiana na Chuo cha Maji na kumpelekea mahakamani.

Sehemu hii ijazwe na Serikali ya Kijij/ Mtaa:

Cheo..... Jina.....

Sahihi..... Mahali..... Tarehe.....

Muhuri wa Serikali ya Kijiji/Mtaa

Orodha ya Viambatanisho vinavyotakiwa kuletwa na mwanafunzi pamoja na fomu ya mkopo:

Tafadhali ambatanisha nakala za vivuli vilivyothibitishwa na **wakili/hakimu** na nyaraka zifuatazo ili kuthibitisha maelezo yako

1. Cheti cha kuzaliwa
2. Cheti cha matokeo ya mtihani ya kidato cha 4
3. Barua ya utambulisho ya mwanafunzi toka Serikali ya Mtaa/ Mjumbe wa nyumba kumi anakotokea
4. Endapo mzazi/wazazi hawapo hai, mwanafunzi aje na cheti/ vyeti cha kifo
5. Endapo mwanafunzi au mzazi ni mlemavu, iletwe barua ya uthibitisho wa Daktari au ustawi wa jamii
6. Endapo mzazi ni mstaafu, Mwanafunzi aje na barua ya kustaafu
7. Pasi ya kusafiria au kitambulisho cha Taifa au kitambulisho cha mpiga kura au kitambulisho cha Mzanzibari mkazi cha **mdhamini**
8. Picha (Passport size) ya mwanafunzi anayeomba mkopo (iandikwe nyuma jina lake pamoja na namba ya usajili ya WI kama ni mwanafunzi anayeendelea, kwa anayeanza aandike jina tu)

NB:

Fomu ya mkopo ambayo itakosa kiambatishi hata kimoja kati ya vilivyoorodheshwa hapo juu itachukuliwa kama fomu batili hivyo haitakuwepo kwenye mchakato wa kupewa mkopo.

MKATABA WA MKOPO KWA MWANAFUNZI – 2017/2018

1. Wahusika wa Mkataba huu

Mkataba huu ni kati ya Bodi ya *The Registered Trustee of the Water Technician Fund*, yenye anwani hapo juu, ambayo ndani ya Mkataba huu itajulikana kama "Bodi" na ..... *(Jina la Mwanafunzi)* ambaye namba yake ya mtihani wa kidato cha Nne ni ..... na ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama Mwanafunzi au Mkopaji

2. Kanuni na Masharti

2.1 Mkataba wa mkopo huu utasainiwa kila mwaka wa masomo. Nyongeza au mafungu ya mkopo ambayo Mkopaji atapewa kila mwaka kwa pamoja yatakuwa sehemu ya Mkataba huu

2.2 Kiasi cha fedha atakachokopeshwa Mwanafunzi kwa mujibu wa Mkataba huu, kitakuwa ni zile fedha zitakazopelekwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Benki ya Mwanafunzi na kile kiasi kitakacholipwa taslimu moja kwa moja kwa Mwanafunzi kupitia Chuo cha maji , na fedha ambazo zitalipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Chuo cha Maji ambazo zitaendelea kulipwa ama kwa Mwanafunzi ama kwa chuo zikihusishwa na gharama za masomo ya Mwanafunzi.

2.3 Mkopo kwa ajili ya ada ya mafunzo italipwa moja kwa moja katika Chuo cha Maji

2.4 Mkopo unaohusu gharama za Mwanafunzi za moja kwa moja utapelekwa kwenye akaunti ya benki ya Mwanafunzi kwa awamu ama atapewa Mwanafunzi kupitia Chuo cha Maji

2.5 Akaunti ya mwanafunzi iliyo katika kumbukumbu za Bodi haitabadilishwa isipokuwa kwa maombi ya Mwanafunzi ambayo yamepitishwa na Chuo cha Maji

2.6 Mwanafunzi ana wajibu wa kujulisha Bodi kuhusu mabadiliko yoyote yale yanayoweza kupelekea kuathiri utoaji au urejeshwaji wa mkopo kwa namna yoyote ile. Mwanafunzi pia ana wajibu wa kuipatia Bodi taarifa nyingine zozote zile zinazohusiana na mkopo wake pale atakapotakiwa kufanya hivyo na Bodi

2.7 Kutokana na mkopo utakaokopeshwa na Bodi, Mwanafunzi anawajibika wakati wote wa kipindi cha masomo yake kuheshimu na kutii sheria ndogo za Chuo cha Maji, Kanuni na maelekezo yatolewayo mara kwa mara na Chuo cha Maji yamejumuishwa katika Mkataba huu kwa marejeo (*for reference*)

2.8 Bodi italazimika kusitisha mkopo kwa Mwanafunzi:

a) Endapo Mwanafunzi atafukuzwa au kushindwa kuendelea na masomo na kutofaulu masomo yake katika Chuo cha Maji

b) Kwa maombi ya Mwanafunzi

c) Endapo mwanafunzi atapuuzia masomo katika Chuo cha Maji

d) Endapo Mwanafunzi atashindwa kuzingatia makubaliano yaliyopo katika kifungu cha **2.7** hapo juu

e) Endapo Mwanafunzi ataacha/ atashindwa kusaini marejesho (returns) za fedha alizolipwa au alizolipiwa kupitia chuoni katika kipindi cha wiki mbili (siku kumi na nne) baada ya kupewa mkopo

f) Endapo mwanafunzi atafariki

g) Kwa sababu nyingine yeyote itakayoonekana na Bodi inafaa

2.9 Endapo itabainika kwamba Mwanafunzi ametoa taarifa za udanganyifu kwa kudhamiria au vinginevyo na taarifa hizo zikapelekea Mwanafunzi kupewa mkopo na Bodi, Bodi itasitisha kumpatia Mwanafunzi sehemu ya mkopo iliyobakia na kiasi chochote cha mkopo kitakachokuwa kimetolewa atatakiwa kukirejesha chote kwa mara moja. Pamoja na kurejesha kiasi chote cha mkopo alichokopeshwa Mwanafunzi kwa mkupuo, Bodi pia itamchukulia Mwanafunzi husika hatua za kisheria

2.10 Mkopo utaanza kurejeshwa mwaka mmoja baada ya mwanafunzi kuhitimu masomo yake toka chuo cha maji

2.11 Kutokana na masharti ya sheria iliyoanzisha Bodi na masharti madogo katika kanuni za mikopo. Mkopo utarejeshwa kwa mafungu kila mwezi au wote kwa pamoja au kwa njia nyingine yoyote ya malipo inayofaa kama itakavyoelekezwa na Bodi

2.12 Bodi itatoa taarifa kuhusu kiasi cha mkopo alichokopeshwa Mwanafunzi kwa kila mwaka wa masomo na jumla ya kiasi kilichoonyeshwa katika taarifa hiyo itakuwa ndicho kiasi anachodaiwa mwanafunzi mpaka mwaka husika. Taarifa hiyo itachukuliwa kuwa sahihi mpaka pale itakapothibitika vinginevyo

2.13 Bodi itakuwa huru kumkopesha kiasi chochote itakachoona kinafaa kulingana na kozi anayosoma na matokeo ya uhitaji wa Mwanafunzi kama itakavyothibishwa na Bodi

2.14 Mkopo huu utatozwa asilimia sita (6%) Kwa mwaka kama gharama ya kuhifadhi thamani ya fedha (value retention fee) zitakazokopeshwa ambazo zitalipwa pamoja na marejesho ya mkopo

2.15 Bodi itakuwa na mamlaka ya kuthibitisha taarifa zinazomhusu mkopaji zilizowekwa katika maombi haya kutoka katika mamlaka yoyote endapo itaona umuhimu wa kufanya hivyo

2.16 Bodi itakuwa na mamlaka ya kuomba na kupokea matokeo ya mitihani moja kwa moja kutoka Chuo cha Maji (WI) ili kuwezesha upangaji wa mikopo ya masomo kwa mwaka unaofuata.

Matamko

Sehemu hii itashuhudiwa na Wakili au Hakimu

1. **Tamko la Mwanafunzi**

Jina kamili: …….....

Anwani ya Posta: …….

Kijiji/Mtaa: …… Kata/Shehia: ……..

Wilaya : …….. Mkoa: …….

Barua pepe: ……..... Namba ya simu ya Mkononi: ……

Mimi ..... Niliye mwanafunzi mkopaji, bila shinikizo lolote na nikiwa na akili timamu nimesoma na kuelewa na kukubali kanuni na masharti ya mkataba huu nikishuhudiwa na aliyesaini hapa chini

Sahihi (ya mwanafunzi):_____ Tarehe: _____

2. **Tamko la Mdhamini (lazima awe mzazi au mlezi wa mkopaji)**

Jina Kamili: ……... Anwani ya Posta: …….

Kijiji/Mtaa: …… Kata/Shehia: …….

Wilaya : ……. Mkoa: ……

Barua pepe: …….. Namba ya Simu ya mkononi: …….

Namba ya kitambulisho cha mpiga kura/ mkazi au Pasi ya kusafiria (Jaza kwa mkono)…….

Mimi..... (Mdhamini) nikiwa na akili timamu bila kulazimishwa, kurubuniwa, ama kushurutishwa na mtu yeyote yule, nathibitisha kwamba nimesoma, kuelewa na kukubali Kanuni na Masharti ya Mkataba huu.

Sahihi: …….. Tarehe: ……

3. **Ushuhuda wa wakili/Hakimu/Mwanasheria**

Imetiwa sahihi na _____ (Jina la mkopaji) ambaye ninamfahamu au ametambulishwa kwangu na _____ ambaye ninamfahamu

Jina Kamili la Wakili/Hakimu/Mwanasheria:_____

Sahihi: …….. Tarehe: ……

Muhuri:

Maelekezo Mengine

1. Andika Jina lako na namba ya usajili na mwaka wa ngazi unayosomea nyuma ya picha kisha bandika panapostahili
2. Tuma fomu iliyosainiwa, kuwekwa picha na viambatanisho vingine ofisi ya RTWTF-Registered trustees of Water technician fund (Hakikisha kuwa fomu yako imepokelewa ofisini)
3. Hakikisha umetoa nakala (copy) ya fomu iliyosainiwa pamoja na viambatisho vyote kabla hujaituma Bodi
4. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya mkopo ni 30 Agost 2017.
5. Hakikisha umelipa ada ya maombi ya sh. 15,000/= kupitia benki ya CRDB:

Jina la akaunti:	**Registered Trustee of the Water Technician Fund**
Benki:	**CRDB**
Namba ya Account:	**0150316425200**

Ukishindwa kutimiza hata sharti moja, maombi yako hayatashughulikiwa.